Mikocheni B,
Coca-Cola Road,
House No.48,
P.O. Box 6166,
Dar es Salaam, Tanzania..

TANGAZO

WITO WA KUWASILISHA MAANDIKO YA MIRADI (PROJECT PROPOSALS) NA DHANA ZA MIRADI (CONCEPT NOTES) ZENYE TIJA KIJAMII NA KIUCHUMI

Taasisi ya SETTA inawatangazia Alumni wa Uturuki Tanzania kuhusu fursa ya kuwasilisha Maandiko ya Miradi (Project Proposals) na Dhana za Miradi (Concept Notes) kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya kijamii.

TAARIFA YA FURSA YA MIRADI

Kuna wafadhili wawili kupitia Ubalozi wa Uturuki ambao wamehitaji kupokea maandiko ya miradi ya maendeleo ya kijamii. Maandiko yanayohitajika ni ya miradi miwili yenye viwango vya juu vya bajeti kama ifuatavyo:

Aina ya andiko	Kiwango cha juu cha bajeti
Mradi wa kwanza (Full Project Proposal)	**USD 150,000**
Mradi wa pili (Full Project Proposal)	**USD 50,000**

DHUMUNI LA WITO WA MIRADI

Lengo ni kuibua mapendekezo ya miradi bunifu, endelevu, na yenye matokeo chanya katika nyanja za maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ambayo yataratibiwa chini ya mwamvuli wa Taasisi ya SETTA.

MAENEO YA VIPAUMBELE (PRIORITY AREAS)

Maandiko yanayowasilishwa yanapaswa kugusa au kujikita katika mojawapo ya maeneo yafuatayo:

1. **Biashara, Uwekezaji na Ujasiriamali:** Miradi inayochochea uanzishwaji au ukuaji wa biashara, minyororo ya thamani, na fursa za ajira kwa Alumni na jamii.

2. **Elimu, Ujuzi na Teknolojia:** Programu za uwezeshaji wa ujuzi, uhamisho wa teknolojia (Technology Transfer), na ushirikiano wa kitaaluma kati ya Tanzania na Uturuki.

3. **Maendeleo ya Kijamii na Afya:** Miradi inayolenga kutatua changamoto za kijamii, kuboresha huduma za afya, na ustawi wa jamii za Watanzania.

4. **Ubunifu na Nishati/Kilimo Endelevu:** Miradi inayotumia mbinu mbadala na bunifu katika kukuza sekta za uzalishaji na hifadhi ya mazingira.

Mikocheni B,
Coca-Cola Road,
House No.48,
P.O. Box 6166,
Dar es Salaam, Tanzania..

VIGEZO VYA UWASILISHAJI NA UHAKIKI (ELIGIBILITY AND CRITERIA)

1. Mwasilishaji wa wazo lazima awe Alumni wa Uturuki aliyesajiliwa katika mfumo rasmi wa Taasisi.
2. Miradi itakayopitishwa itatekelezwa na kusimamiwa chini ya miongozo na usimamizi wa Taasisi.
3. Mradi lazima uonyeshe kwa uwazi tija ya kiuchumi/kijamii, matokeo tarajiwa, walengwa wa mradi, na mpango wa uendelevu (Sustainability Plan).

MUUNDO WA ANDIKO

1. **Concept Note:** Andiko lieleze muhtasari wa tatizo, suluhisho, walengwa, bajeti ya makadirio, na matokeo.
2. **Full Project Proposal:** Andiko lijumuishe maelezo ya mradi, mpango kazi, uchambuzi wa hatari, bajeti ya kina, na tathmini.

NJIA NA TAREHE YA MWISHO YA KUWASILISHA

1. **Format ya Files:** Maandiko yote yawasilishwe katika mfumo wa PDF au MS Word.
2. **Anwani ya Barua Pepe:** Maandiko yatumwe kwenda: proposal@settafoundation.or.tz

   Weka nakala kwa “Cc”: info@settafoundation.or.tz
3. Kichwa cha Barua Pepe (Subject Line): SETTA PROJECT PROPOSAL 2026 - [Jina la Mradi]
4. Tarehe ya Mwisho: Tarehe 12 Disemba, 2026, Saa 5:59 Usiku.

HATUA ZITAKAZOFUATA (SELECTION PROCESS)

Hatua	Maelezo	Muda tarajiwa
Hatua ya 1	Kupokea na uhakiki wa awali wa maandiko (Screening)	09.11.2026 – 12.12.2026
Hatua ya 2	Usaili na uwasilishaji wa miradi iliyochaguliwa (Shortlisting)	13 – 19.12.2026

Mikocheni B,
Coca-Cola Road,
House No.48,
P.O. Box 6166,
Dar es Salaam, Tanzania..

MAWASILIANO NA UFAFANUZI

Kwa ufafanuzi au maswali kuhusu wito huu, tafadhali wasiliana na Kamati ya Uratibu wa Miradi kupitia:

- **Simu:** +255 710 999 989.

"Tukishirikiana, Tunajenga Jamii Yenye Tija na Uhusiano Imara."

"Kuimarisha Uhusiano wa Tanzania na Uturuki kupitia Utaalamu, Uvumbuzi na Maendeleo Endelevu."

Imetolewa na:
Kamati ya Uratibu wa Miradi,
Taasisi ya SETTA.
Tarehe: 09 Novemba, 2026.

SOCIAL ECONOMIC TIER OF TURKISH ALUMNI (SETTA) P. O. BOX 6166 DAR ES SALAAM – TANZANIA